CHILDREN'S DIGNITY FORUM
CDF
UTU WA MTOTO

FORWARD
Safeguarding rights & dignity

"SIKUJUA NI KWA NAMNA GANI NILIPATA MIMBA"

Utafiti Shirikishi kuhusu Mimba na Kuwa Mama katika umri mdogo uliofanywa Wilaya ya Mpwapwa, Tanzania

MUHTASARI WA RIPOTI

FEBRUARI, 2018

Imechapishwa mwaka 2018 na Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) and FORWARD (Foundation for Women's Health, Research & Development). Haki miliki Februari 2018 Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) and Foundation for Women's Health, Research & Development (FORWARD).

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyoye ya chapisho hili (ikiwa ni pamoja na picha) inayoweza kutolewa, kuhifadhiwa katika mfumo wowote, kusambazwa, au kurudufishwa kwa aina ama njia yoyote, ikiwa pamoja na kunakili, kurekodi au njia nyingine ya elektroniki, njia za kiufundi bila ruhusa iliyotolewa mapema kwa maandishi na wachapishaji, ila tu pale inaponukuliwa kwa kifupi, ama kudokezwa kwenye makala.

Waandishi: Dorothea Ernest, Naana Otoo-Oyortey, Seblework Belay Gebreegziabher, Koshuma Mtengeti.

Imefadhiliwa na: Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida) na The Sigrid Rausing Trust.

SWEDEN

SIGRID RAUSING TRUST

YALIYOMO

SHUKRANI.....05

KUKABILIANA NA MIMBA ZA UTOTONI TANZANIA 07

MADHUMUNI YA UTAFITI 07

MBINU YA UTAFITI SHIRIKISHI (PEER) 10

MATOKEO YA UTAFITI 13

UZOEFU WA WASICHANA KUHUSU MIMBA KATIKA MAZINGIRA YA SHULE 13

UMASKINI UNACHANGIAJE 15

ELIMU.....16

KUKOSEKANA KWA MAJUKUMU YA KIFAMILIA 16

ELIMU DUNI YA NYUMBANI KUHUSU JINSIA NA MAHUSIANO.....17

NGONO MALIPO 17

UKOSEFU WA TAARIFA NA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI 18

MAPENDEKEZO 19

HITIMISHO 22

SHUKRANI

Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) na FORWARD wanapenda kutoa shukrani kwa Watafiti na Wasimamizi wa Utafiti Shirikishi (PEER) waliotoa muda wao, juhudi, shauku na mnyenyekeo wa dhati katika utafiti huu. Bila dhamiri yao ingekuwa vigumu kufanikiwa katika utafiti huu. P ia, t unapenda k uwashukuru wafanyakazi wa shirika la CDF, Clara Wisiko na Evans Rwamuhuru ambao walikuwa wawezeshaji na kutoa msaada wakati wa mafunzo na ukusanyaji wa taarifa.

Tunatambua juhudi zilizofanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la CDF, Koshuma Mtengeti kwa kutoa msaada wakati wa kusanifu, kuchanganua taarifa na uandishi wa ripoti ya mwisho ya utafiti huu. Tunatoa shukrani za dhati kwa wafanyakazi wote wa shirika la CDF hasa Lennyster Byalugaba, Sophia Temba, Gloria Mbuya, Frederick Baragwiha, Kambibi Kamugisha, Nancy Minja, Amina Ally na Michael Jackson ambao wamekuwa msaada mkubwa wakati wote wa utafiti huu.

Shukrani za kipekee zimwendee Dorothea Ernest kwa kusimamia utafiti huu Shirikishi (PEER), uchanganuzi wa taarifa na uandishi wa ripoti ya mwisho. Shukrani nyingi ziende kwa Naana Otoo-Oyortey, Mkurugenzi Mtendaji , Seblework Belay Gebreegziabher, Afisa wa Programu , Adwoa Kwateng-Kluvitse, Mkuu wa Kitengo cha Utetezi, na Naomi Reid, Meneja wa Mawasiliano na Matukio (wote kutoka shirika la FORWARD) kwa kutoa msaada wa kiufundi na uhariri, pamoja na uhakiki wakati wote wa mchakato wa utafiti.

Pia, CDF inawashukuru sana FORWARD kwa msaada wa kiufundi, usanifu na uhariri.

Mwisho kabisa, utafiti huu umewezeshwa kwa msaada mkubwa wa fedha kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (Sida) na Mfuko wa Udhamini wa Sigrid Rausing Trust. Shukrani nyingi ziwaendee kwa dhamiri yao ya dhati ya kusaidia kazi zetu.

“KWENYE JAMII YANGU, UKIPATA MIMBA FAMILIA INAKUDHARAU. TUNAHITAJI WATUTUNZE, WATUPENDE NA WATOE MSAADA KWA WASICHANA NA WASICHANA WALIOPATA MIMBA KATIKA”

KUKABILIANA NA MIMBA ZA UTOTONI TANZANIA

MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuongeza maarifa na uelewa kuhusu hali ya mimba za utotoni na wasichana waliozaa katika umri mdogo katika Wilaya ya Mpwapwa, Tanzania kwa kujikita hasa kwenye masuala yafuatayo:

- Kupata taarifa muhimu za kuongeza ufahamu katika mapambano ya kukomesha mimba za utotoni na kuzaa katika umri mdogo, na kupaza sauti za wasichana na wanawake vijana walioathirika kwa kutumia mchakato wa utafiti huu;
- Kuchunguza uzoefu na mitazamo ya wasichana na wasichana waliopata mimba katika umri mdogo na kuelewa changamoto wanazokabiliana nazo kwenye maisha yao;
- Kutambua mitazamo ya jamii na vijana kuhusiana mimba za utotoni, wasichana waliopata mimba katika umri mdogo na kujihusisha na ngono katika umri mdogo;
- Kutathimini uzoefu wa wasichana katika huduma na sera zilizopo zinazohusu afya ya uzazi, mimba za utotoni na uzazi katika umri mdogo.

Mimba na ndoa za utotoni ni mojawapo ya changamoto kubwa za kiuchumi na kijamii zinazoikabili Wilaya ya Mpwapwa, iliyo Mkoa wa Dodoma, Tanzania. Kuwapa mimba wasichana katika umri mdogo kabla ya ndoa, na wakati mwingine kuwalazimisha kuolewa bila ridhaa yao inasababisha kuwepo kwa majanga ya kiuchumi na kijamii nchini. Tatizo hili linazuia fursa na ndoto za wasichana sanjari na kusababisha umasikini endelevu na kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia.

Vijana wanakosa elimu kuhusu ngono salama na miili yao na matokeo yake hujihusisha na ngono zembe. Hii ni kwa sababu ya kushindwa kuwaelimisha wasichana walioko shuleni na kwenye jamii kuhusu masuala ya ngono na haki zao. Unyanyasaji wa kingono, ngono malipo na hisia za wasichana kuamua kujihusisha na ngono malipo ili kujikimu kimaisha vina uhusiano mkubwa na uwepo wa mimba nyingi za utotoni.

Wazazi wanaonekana kutotimiza majukumu yao vyakutosha kwa wasichana na wanawake vijana, si kwamba tu wanashindwa kuelimisha binti zao juu ya ngono na miili yao, lakini kwa sababu wanashindwa kuwasaidia binti zao wanapopata mimba. Wasichana waliopata watoto katika umri mdogo hufukuzwa katika familia zao kwani huchukuliwa kuwa wamewaaibisha wazazi wao.

Wakati huo huo, kuwapeleka wasichana shule si kipaumbele kwa familia zinazodhani si utamaduni wao. Wasichana wanaonekana kuwa wanafaa zaidi kuwa nyumbani, shambani, au kuwa hakuna haja ya kuwasomesha kwa kuwa wataolewa punde.

Matamko na sera za Serikali kuwa wasichana wasirudi shule baada ya kupata mimba yanamaanisha kuwa wasichana ambao ni waathirika wa mimba za utotoni na wasichana waliopata watoto katika umri mdogo wabaki kuwa maskini, yamkini hata kujihusisha kwenye mzunguko wa ngono malipo ili waweze kujikimu sambamba na kuwahudumia watoto wao.

Maarifa duni na ukosefu wa huduma za afya ya uzazi katika ngazi za chini huongeza tatizo, husababisha wasichana wengi wasiwe na uelewa pamoja na kutopata huduma hizo. Hakuna huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana katika ngazi za wilaya na kata na huduma zilizopo hazijawalenga vijana. Upatikanaji wa huduma hizi sio kipaumbele ambapo huwaacha wasichana kuwa wahanga wa ndoa za utotoni na kuharibu ndoto zao.

Haipaswi kuwa hivi.

Utafiti huu shirikishi (PEER) uliofanywa Wilaya ya Mpwapwa unaonesha kwamba wasichana na wanawake vijana wanajua hali yao, kama vile sababu za mimba na kupata watoto katika umri mdogo na nini kifanyike katika kutatua tatizo hili.

Hivyo wanatoa wito wa kubadili mtazamo kuhusu wasichana, kuboresha upatikanaji wa elimu rasmi na huduma za afya ya uzazi pamoja na kusaidiwa na wazazi wao na wasichana wenzao (kupitia klabu za wasichana).

Wasichana wanajua kwamba wao na familia zao wakijielewa na kukwamuliwa kutoka katika umasikini maisha yao yanaweza kuboreka na kupunguza mimba za utotoni.

Zaidi ya yote, wanatoa wito wa kupatiwa msaada wa elimu ya ujasiriamali. Wanatambua kuwa wasichana wanaopata mimba, kurudi shule ni kipaumbele kwao. Kwa wale ambao hawawezi kurudi shule, msaada unahitajika ili waweze kuanzisha biashara ndogondogo zitakazowawezesha kupata kipato cha kujikimu kimaisha.

Wasichana, wanawake na wanaume vijana walioshiriki katika utafiti shirikishi (PEER) wana matumaini ya mustakabali wao. Wanaamini kuwa utatuzi upo ila jitihada zaidi zinahitajika ili kutokomeza umaskini, mimba na ndoa za utotoni.

Mimba za utotoni Tanzania na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa ujumla ni tatizo kubwa. Kutokana na takwimu za utafiti wa demografia na Afya Tanzania za mwaka 2015-16, 27% ya wanawake vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wameanza kuzaa, 21% wameshazaa, na 6% zaidi wana mimba za watoto wao wa kwanza. Mimba za utotoni pia zinaongezeka Tanzania: 26% ya wasichana walizaa au walikuwa na mimba mwaka 2004-05, baadae idadi ilipungua na kuwa 23% mwaka 2010, kisha ikaongezeka na kuwa 27% mwaka 2015-16. Hali hii inatia wasiwasi sana kwa maendeleo ya nchi.

Huko Dodoma zaidi ya nusu (51%) ya wanawake vijana wameathiriwa na ndoa za utotoni, na zaidi ya theluthi (39%) wameathiriwa na mimba za utotoni (URT, TDHS – MIS 2015/16). Watoto walio kwenye mkoa huu wanakabiliwa na changamoto za kijamii, kiuchumi na kiafya kutokana na matatizo haya.

Katika Wilaya ya Mpwapwa ambako utafiti huu ulifanyika, mwaka 2016, wasichana 48 (1.25% ya watoto walioacha shule) waliacha wakiwa sekondari na wasichana watano (10% ya jumla ya walioacha shule) waliacha wakiwa shule ya msingi kwa sababu ya mimba. Taarifa kutoka Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa zinaonesha kwamba mwaka 2016 wasichana walio chini ya umri wa miaka 20 walikuwa 26% ya wazazi wote, wengi wakiwa na umri kati ya miaka 14 hadi 17.[1] Vilevile, taarifa za hospitali ya taifa zinaonyesha kuwa wasichana walio chini ya miaka 20 ambao ni takribani 40% ya wazazi wote waliozaa kwa njia ya upasuaji mwaka 2016. kwani wakina mama watoto wengi hawawezi kuzaa kwa njia ya kawaida.[2]

[1&2] CDF (2017) Ripoti ya Utafiti wa Awali, Wilaya yaTarime na Mpwapwa

MBINU YA UTAFITI SHIRIKISHI (PEER)

Utafiti huu ulitumia njia ya kushirikisha wanajamii wenyewe kukusanya taarifa katika jamii yao [Participatory Ethnographic Evaluation Research (PEER)]. Hii imewezesha kupata taarifa katika jamii na makundi ya watu ambao wasingeweza kutoa taarifa nyeti zinazowahusu wao wenyewe au jamii zao kwa mtu mgeni ambaye hawana mazoea naye. Imetumia wanajamii waliochaguliwa na wanaohusika moja kwa moja na suala linalotafitiwa kuhusika na mchakato wa utafiti. Wanajamii waliochaguliwa walipewa mafunzo ya mbinu za ukusanyaji wa taarifa kwa weledi kutoka kwa marafiki zao ndani ya jamii.

Jumla ya Watafiti shirikishi 16 wa PEER (wasichana waliopata watoto katika umri mdogo 12 na wavulana 4) wenye umri kati ya miaka 14 hadi 17 walichaguliwa kutoka kata nne za Wilaya ya Mpwapwa ambazo ni Kibakwe, Mpwapwa Mjini, Berege na Pwaga. Watafiti hawa wa PEER walikuwa na wasimamizi wanne, mmoja kutoka kila kata, ambao walikuwa ni walimu.

Kabla ya ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wenzao, watafiti shirikishi walipewa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa siku tatu ili kuwapatia stadi za msingi za ukusanyaji wa taarifa na kudodosa. Baada ya hapo, watafiti shirikishi walikwenda kuwahoji wenzao kwa kutumia maswali yaliyogawanywa katika mada kuu tatu: (1) hali ya maisha ya Wilaya ya Mpwapwa; (2) sababu za mimba za utotoni na uzazi katika umri mdogo (3) mapendekezo makuu katika kushughulikia changamoto wanazozipata wasichana wilayani Mpwapwa.

> **"UTAFITI SHIRIKISHI UMENIONGEZEA UWEZO WA KUELIMISHA WASICHANA WENZANGU HAPA KIJIJINI JUU YA MADHARA YA MIMBA ZA UTOTONI NA WALIJADILIANA NAMI KUHUSU SABABU YA KUPATA MIMBA ZA UTOTONI. PIA, NIMEWEZA KUWAPA TUMAINI KWAMBA KUPATA MIMBA UTOTONI SIO MWISHO WA MAISHA."**

“BINAMU YANGU ALIPATA FISTULA ALIPOKUWA ANAJIFUNGUA, ALIPATA MIMBA AKIWA MDOGO”

MATOKEO YA UTAFITI

Walipoulizwa juu ya madhara ya mimba na kuwa mama katika umri mdogo, washiriki walizungumzia kuhusu kuacha shule, matatizo wakati wa kujifungua, fistula*, kutoweza kutimiza wajibu wa kuwa mzazi na wasichana kutegemea zaidi familia zao.

"MSICHANA ANAWEZA KUPATA MATATIZO WAKATI WA KUJIFUNGUA NA MARA NYINGINE WAZAZI WAKE HAWANA FEDHA ZA KUMPELEKA HOSPITALI NA ANAISHIA KUJIFUNGULIA NYUMBANI AMBAPO HUWEZA KUSABABISHA KIFO CHA MAMA NA MTOTO."

"KWA MFANO, NAHITAJI KUTIMIZA MAHITAJI YA MWANANGU, ANAPOUMWA NATAKIWA NIMPELEKE KLINIKI. HII NI NGUMU KWANGU KWANI SINA CHANZO CHOCHOTE CHA MAPATO."

UZOEFU WA WASICHANA KUHUSU MIMBA KATIKA MAZINGIRA YA SHULE

Walipoulizwa juu ya huduma za afya ya uzazi zinazopatikana shuleni, washiriki wengi walisema kwamba hazipo. Hii ni pamoja na ukosefu wa mitaala ya shule na mwongozo kuhusu elimu juu ya afya ya uzazi kwenye shule nyingi za Tanzania na hususani kwenye jamii za vijijini.

"HAKUNA ELIMU YOYOTE YA AFYA YA UZAZI ILIYOTOLEWA KWENYE SHULE NILIYOSOMA, HATUJUI CHOCHOTE JUU YA SUALA HILI. HATUKUFUNDISHWA JUU YA AFYA YA UZAZI. MIMI MWENYEWE NILIJUA BAADA YA KUPATA MAFUNZO KUTOKA CDF."

"HAKUNA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI WALA MAARIFA WALIYOFUNDISHWA WANAFUNZI NA WALIMU WA SHULE YANGU YA ZAMANI. NILIANZA KUSIKIA KUHUSU AFYA YA UZAZI KUTOKA KWA RAFIKI ZANGU NYUMBANI."

** Fistula hutokea wakati wa uchungu pinzani ambapo kichwa cha mtoto hukaa nyongani kwa mama kwa muda mrefu. Upatakani wa damu kwenye nyama zinazozunguka kibofu cha mkojo, mrija wa mkundu na uke hukosekana na kusababisha nyama hizo kuharibika na kutengeza shimo kati ya uke na kibofu au mrija wa mkundu. Hii husababisha mtu asiweze kushikilia haja. Mara nyingi mtoto haponi.*

Msichana alipogundulika kuwa ni mjamzito, washiriki walisema kuwa hakuweza kupata huduma na taarifa za kutosha za afya ya uzazi.

“KATIKA SHULE YETU, HAPAKUEPO NA HUDUMA YA USHAURI NASIHI BAADA YA KUTHIBITIKA KUWA MWANAFUNZI NI MJAMZITO, WANAKUKAMATA NA KUKUPELEKA KATIKA KITUO CHA POLISI. BAADA YA HAPO WANAKULAZIMISHA KUMTAJA ALIYEKUPA UJAUZITO ILI AWEZE KUKAMATWA.”

“HAKUNA HUDUMA YA USHAURI NASIHI INAYOTOLEWA SHULENI, NJIA PEKEE WANAKURUDISHA KWA WAZAZI NA INAKUA NI MWISHO WA MASOMO YAKO”

“WALE WALIOGUNDULIKA KUWA WANA MIMBA SHULENI KWETU WALIFUNDISHWA DHIDI YA MADHARA YA KUTOA MIMBA, KWAMBA KUTOA MIMBA KUNAWEZA KUSABABISHA UHARIBIFU WA VIUNGO VYA UZAZI NA MARA NYINGINE KIFO.”

UMASKINI UNACHANGIAJE

Wazazi wanaoishi katika umasikini wanahangaika kupata mahitaji ya watoto wao, na suala la kuwapeleka shule huonekana ni gharama kubwa kwao. Wazazi huweza kuamua kuwaoza binti zao ili waondokane na majukumu ya kuwahudumia. Kivutio kingine ni 'mahari' ambayo familia ya msichana huipata kutoka kwenye familia yake mpya. Matokeo mengine ya umaskini ni kwa wasichana kulazimika kujihusisha na ngono malipo ili wapate vifaa vya shule na vitu vingine ambavyo wazazi hawavimudu.

"WASICHANA NA WANAWAKE HAWANA SHUGHULI MAALUMU ZA KUJIINGIZIA KIPATO, WANATEGEMEA ZAIDI KILIMO, AMBACHO SI CHA KUAMINIKA KUTOKANA NA MABADILIKO YA MVUA MARA KWA MARA ."

"WAZAZI HUSHINDWA KUWAPATIA WATOTO WAO MAHITAJI MUHIMU KAMA VILE NGUO NA CHAKULA, AMBAPO HALI HII HUSABABISHA WASICHANA KURUBUNIWA KWA URAHISI NA WANAUME. KWA MFANO, MSICHANA ANAPOKOSA PESA AU VIATU NI RAHISI SANA KWAKE KUSHAWISHIWA NA MWANAUME NA KUJIINGIZA KWENYE NGONO ILI KUPATA MAHITAJI HAYO.

"MAISHA YA KILA SIKU HAPA KIBAKWE NI MAGUMU SANA, MAISHA NI MAGUMU SANA HASA PALE UNAPOKUWA NA MTOTO, INAKUWA NGUMU KUMPATIA MAHITAJI YA MSINGI. KWA MFANO, NILIPATA MIMBA NIKIWA NA UMRI WA MIAKA 16, HII ILITOKANA NA KUJIHUSISHA NA VITENDO VYA NGONO NA WANAUME WALIONIZIDI UMRI ILI NIPATE PESA."

ELIMU

Wazazi wanaoishi katika umaskini wanapata shida kutimiza mahitaji ya watoto wao, na kuwapeleka shule huwa ni gharama. Wazazi huweza kuamua kuwaoza binti zao ili waondokane na majukumu. Kivutio kingine ni 'mahari' ambayo familia ya msichana huipata kutoka kwenye familia yake mpya. Matokeo mengine ya umaskini ni kwa wasichana kulazimika kuingia kwenye ngono ya kulipwa ili wapate vifaa vya shule na vitu vingine ambavyo wazazi hawavimudu.

"KATIKA JAMII YETU, WAVULANA WANAPEWA KIPAUMBELE KATIKA SUALA LA ELIMU KULIKO WASICHANA. WATU KATIKA JAMII YETU WANASEMA KWAMBA WASICHANA HAWANA UWEZO WA KUCHANGIA KATIKA MAENDELEO YA TAIFA AU KUWA VIONGOZI."

"KUNA WAZAZI WAMEKUWA WAKIWAMBIA BINTI ZAO KUWA HAWANA PESA ZA KUWAPELEKA SHULE NA KWAMBA KUWAELIMISHA SIO MUHIMU KWANI WATAISHIA KUOLEWA TU."

"KATIKA JAMII YANGU WATU WANAAMINI KUWA KUMUELIMISHA MSICHANA NI KUPOTEZA RASILIMALI NA FEDHA KWANI ATAOLEWA NA FAMILIA NYINGINE."

"PIA, WASHIRIKI WALISEMA KUWA HAWAJAWAHI KUMUONA MSICHANA ALIYEPATA MIMBA NA BAADAE AKAFANIKIWA KARUDI NA KUENDELEA NA SHULE, TAKRIBANI WOTE WALIKUTWA WAKILEA WATOTO WAO NA WALITEGEMEA KWAMBA MAMBO YATABADILIKA MUDA MFUPI UJAO."

FAMILIA KUTOJALI

Utafiti umeonyesha kuwa wasichana wengi waliachiwa mzigo wa kulea watoto peke yao maana mara nyingi hutelekezwa na baba wa watoto hao. Wengine hukosa msaada kutoka kwa wazazi wao na ndugu wa karibu kwa sababu huonekana kuwa wameziaibisha familia zao. Ili waweze kuishi, baadhi ya wakina mama waliozaa katika umri mdogo walisema kwamba inabidi wajihusishe na ngono malipo ili waweze kupata fedha za kujikimu. Baadhi ya washiriki walisema kuwa 'uvivu' wa wazazi wao kwenda kufanya kazi, kushindwa kuwasaidia kutimiza majukumu yao imekuwa ni sababu iliyowashawishi binti zao kujihusisha na ngono malipo ili wapate fedha.

"UMASKINI KWENYE JAMII YA KIBAKWE UNASABABISHWA NA UVIVU, WATU HAWAPENDI KUFANYA KAZI AU KUJIHUSISHA NA SHUGHULI YOYOTE INAYOWEZA KUWAINGIZIA KIPATO. VIJANA WENGI HUPENDA KUKAA NYUMBANI BILA KUJIHUSISHA NA SHUGHULI YOYOTE AU HUJIUNGA NA MAKUNDI YASIYO NA TIJA BADALA YA KUJISHUGULISHA NA KAZI ZA UZALISHAJI"

"KWA UJUMLA MAISHA NI MAGUMU SANA, WAZAZI WANASHINDWA KUTOA MAHITAJI YA MSINGI KWA WATOTO WAO."

"HUKU BEREGE, UMASKINI UNASABABISHWA NA UVIVU WA WAZAZI, MAANA WENGI HAWAFANYI KAZI. WAZAZI WANAENDEKEZA ULEVI BILA KUJALI WATOTO WAO, HASA WASICHANA NA MATOKEO YAKE WATOTO WAO HUSHINDWA KUPATA MAHITAJI YA MSINGI, NA HATIMAYE HUSHAWISHIKA KUJIHUSISHA NA VITENDO VYA NGONO AMBAVYO HUHATARISHA MAISHA MAISHA YAO."

UDUNI WA ELIMU ITOLEWAYO NYUMBANI KUHUSU JINSIA NA MAHUSIANO

Kwa wasichana wengi, ukosefu wa taarifa sahihi, majadiliano ya wazi au mwongozo wa wazazi huchangia kuongezeka kwa hatari ya kupata mimba maana hawana nafasi ya kujifunza au kujadili juu ya masuala ya afya ya uzazi. Mambo haya yanaonekana kuwa ni miiko.

"SIFAHAMU LOLOTE KUHUSU HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, WAZAZI WANGU WANAONA AIBU KUZUNGUMZA NA MIMI JUU YA MASUALA YA NGONO."

"SABABU KUBWA INAYOSABABISHA MIMBA ZA UTOTONI NA KUWA MAMA KATIKA UMRI MDOGO NI UKOSEFU WA MATUNZO KUTOKA KWA WAZAZI. WAZAZI WENGI KWENYE JAMII ZETU HAWANA MUDA NA WATOTO WAO."

"WATOTO HAWANA TAARIFA NA ELIMU YA KUTOSHA JUU YA NINI WAFANYE ILI WASIPATE MIMBA. PIA, WAZAZI HAWANA MUDA WA KUZUNGUMZA NA WATOTO WAO KUHUSU MAADILI NA TABIA HATARISHI. TANGU NILIVYOVUNJA UNGO, MAMA YANGU HAKUWAHI KUNIFUNDISHA CHOCHOTE. HIVYO, SIKUJUA KWAMBA NIKIJIHUSISHA NA NGONO NAWEZA KUPATA MIMBA."

NGONO MALIPO

Mimba nyingi za utotoni zinasababishwa na wanaume wanaowalazimisha wasichana kufanya nao ngono, kwa ahadi ya kuwapa fedha endapo watakubali. Kutokana na hali ngumu ya kiuchumi, baadhi ya wasichana hukubali kufanya ngono bila kutumia kinga. Hata hivyo, hali hii hutokana na nguvu waliyonayo wanaume, watu wazima wanaowatongoza wasichana kwa ushawishi wa pesa.

"MIMBA ZA UTOTONI HUSABABISHWA NA WANAUME WANAOWATONGOZA WASICHANA NA KUWAAHIDI KUWAPATIA FEDHA ENDAPO TU WATAKUBALI KUFANYA NAO NGONO"

"BAADHI YA WASICHANA HAWANA SARE ZA SHULE, NA MWANUME ANAWEZA KUMUAHIDI KUWA ATAMPATIA SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE . KWAHIYO IKIFIKIA HAPO, MSICHANA HANA JINSI ZAIDI YA KUKUBALI KUFANYA NAE NGONO ILI APATE MAHITAJI YAKE"

"WASICHANA WENGI WANAOJIHUSISHA NA BIASHARA YA NGONO WANADHANI KUWA BIASHARA HIYO NI RAHISI MAANA HAIHITAJI UWE NA UWEZO WA KIFEDHA/MTAJI AMBAPO SHUGHULI NYINGINE KAMA VILE BIASHARA NDOGO NDOGO ZINAHITAJI MTAJI AMBAO NI CHANGAMOTO KWA WASICHANA"

UKOSEFU WA TAARIFA NA HUDUMA YA UZAZI WA MPANGO

Wasichana wanakosa hata taarifa za msingi kuhusu miili yao, balehe, afya ya uzazi na hawapati ushauri wa kutosha kuhusu uzazi wa mpango na huduma husika. Uelewa mdogo na upatikanaji duni wa huduma rafiki za afya ya uzazi zinazojali vijana zimechangia kuwepo kwa mimba za utotoni, kuzaa katika umri mdogo na utoaji wa mimba maana vijana wanamsukumo mkubwa wa kujihusisha na ngono, lakini hawana rasilimalli za kuwasadia au kukabiliana na madhara yake. Walipoulizwa juu ya ufahamu wa huduma za afya ya uzazi washiriki wengi walisema kwamba wanahitaji kujua zaidi kuhusiana na masuala ya afya ya uzazi na walikuwa na shauku kubwa ya kuzipata huduma hizo.

"MIMI NI MAMA NILIYEZAA KATIKA UMRI MDOGO, NILIPATA MIMBA KWA SABABU SIKUJUA NILICHOKIFANYA NA SIKUFAHAMU ATHARI ZA KUJIHUSISHA NA VITENDO VYA NGONO KATIKA UMRI MDOGO"

"UKOSEFU WA ELIMU YA AFYA HUSABABISHA MIMBA ZA UTOTONI KWANI WASICHANA HAWAJUI JINSI YA KUJIKINGA NA MIMBA."

"BAADHI YA WANAWAKE NA WASICHANA KWENYE JAMII YETU HUTUMIA KAMBA KUZUIA MIMBA. MSICHANA MMOJA ALISEMA KUWA BIBI YAKE ANAWEZA KUMVISHA KAMBA KIUNONI NA AKAJIKINGA NA MIMBA."

"HUDUMA HAZIPATIKANI KWA WOTE KUTOKANA NA UMBALI WA KUFIKA KITUO CHA AFYA, NA UELEWA MDOGO KUHUSU AFYA YA UZAZI MIONGONI MWA WATOA HUDUMA ZA AFYA"

MAPENDEKEZO

Washiriki wa utafiti huu walitoa mapendekezo mbalimbali ya afua zinazoweza kutatua changamoto zinazowakabili wasichana na wanawake walioolewa katika umri mdogo:

Msaada wa Serikali kwa akina mama waliozaa katika umri mdogo, ili waweze kuendelea na masomo bila ya kuonewa au kunyimwa fursa ya kupata elimu. Wasichana wengi walitaka wapewe nafasi nyingine ili kuboresha maisha yao kwa kupatiwa elimu.

> "KULIKUWA NA MSICHANA KIJIJINI KWETU ALIYEACHA SHULE KWA SABABU ALIKUWA NA UJAUZITO. BAADA YA KUJIFUNGUA, WAZAZI WAKE WALIMPELEKA SHULE BINAFSI AMBAKO ALIENDELEA NA MASOMO YAKE"

> "WAZAZI WANGU WALIJISIKIA VIBAYA SANA BAADA YA KUGUNDUA KUWA NINA UJAUZITO, LAKINI WALINIONYA NISIRUDIE TENA NA WALINISAIDIA WAKATI NINA MIMBA, HADI SASA WANAENDELEA KUNISAIDIA KUMPATIA MTOTO WANGU MAHITAJI MUHIMU"

Huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana, na uboreshaji uelewa wa wanajamii juu ya huduma hizo.

> "WAVULANA NA WASICHANA INABIDI WAELIMISHWE JUU YA AFYA YA UZAZI, HASA KUHUSU ATHARI ZA MIMBA ZA UTOTONI"

> "WASICHANA WALIO SHULENI WANAHITAJI KUWA NA UELEWA WA KUTOSHA KUHUSU HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA UZAZI WA MPANGO. NI LAZIMA WAFUNDISHWE NAMNA YA KUTUMIA HUDUMA HIZO"

> "HUDUMA ZILIZOPO SI RAFIKI, TUNAHITAJI HUDUMA RAFIKI AMBAPO TUNAWEZA KUZUNGUMZIA MASUALA YETU KWA UHURU. NADHANI TUNAHITAJI MTU WA RIKA LETU ILI TUWE HURU KUZUNGUMZA. TUNAPOKWENDA KWENYE VITUO VYA AFYA, TUNAKOSA UHURU NA TUNAKUWA NA AIBU KUZUNGUMZA NA MUUGUZI"

Uchaguzi wa kurudi shule. Washiriki walizungumza kwa msisitizo mkubwa juu ya haja ya wasichana waliozaa katika umri mdogo kupatiwa fursa ya kurudi shule.

> **"WASICHANA NA VIJANA WA KIKE WALIOPATA MIMBA KATIKA UMRI MDOGO WANATAKA KULETA MABADILIKO HAPO BAADAE KWA KURUDI SHULE MARA TU BAADA YA WATOTO WAO WATAKAPOKUA. MSICHANA MMOJA ALISEMA, "MTOTO WANGU AKIFIKISHA MIAKA MIWILI, NITARUDI SHULE"**

> **"WASICHANA WALIOZAA KATIKA UMRI MDOGO WANATOA WITO KWA SERKALI NA WAZAZI KUWASAIDIA ILI KUTIMIZA/KUFIKIA NDOTO ZAO"**

Msaada wa fedha na stadi za ujasiriamali, ikiwemo jitihada za vitendo zaidi kutoka serikalini na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuwasaidia wasichana na wanawake waliozaa katika umri mdogo kurudi shuleni,au kujihusisha na biashara ndogondogo.

> **"NINAJISHUGHULISHA NA UUZAJI WA MAANDAZI HAPA KIKIJINI. PESA NINAZOZIPATA KUTOKANA NA BIASHARA YANGU NAZITUMIA KWA AJILI YA KUENDESHA MAISHA YANGU SANJARI NA KUMLEA MWANANGU"**

> **"NINENUNUA ARDHI EKARI MOJA, NA NINALIMA MAHINDI, MTAMA NA KARANGA, KUTOKANA NA HILI, NINAWEZA KUJIKIMU MIMI NA MWANANGU"**

> **"WASICHANA WANAHITAJI MIKOPO MIDOGO MIDOGO ILI WAWEZE KUANZISHA BIASHARA NDOGO NDOGO KAMA VILE KUUZA NYANYA, MITUMBA NA MBOGA ZA MAJANI"**

Uanzishwaji wa klabu za wasichana. Kuna haja ya kuwa na sehemu salama kwa ajili ya wanawake waliopata mimba katika umri mdogo kujadiliana, kuelimishana na kusaidiana juu ya masuala ya ngono, uzazi wa mpango, ukatili wa kijinsia, na changamoto maalumu zinazowakabili katika jamii. Wasichana na akina mama waliopata mimba katika umri mdogo ambao wanashiriki kwenye shughuli hizi wanaweza kujijengea uwezo na kuwa mawakala wazuri wa mabadiliko kwenye jamii zao.

> **"SISI KAMA WASICHANA TUNACHUKULIWA KUWA NI WAATHIRIKA WA HALI ILIVYO. TUKIKUSANYIKA PAMOJA KAMA KIKUNDI TUTAKUWA NA UJASIRI NA KUIMARIKA, NA KUTIANA MOYO MIONGONI MWETU NA KUWAFIKIA NDOTO ZETU"**

> **"TUNA VIKUNDI VYA WANAWAKE KWENYE JAMII YETU NA VINAWASAIDIA WANAWAKE KIUCHUMI. KAMA TUKISAIDIWA KUANZISHA KIKUNDI NAAMINI ITATUSAIDIA NA SISI"**

Wajibu mkubwa kwa wazazi na msaada wao katika kuwapatia taarifa za afya ya uzazi pamoja na mahitaji ya msingi ya wasichana ili wabaki shule. Pia, wazazi wanahitaji kujifunza jinsi ya kuwasaidia wasichana waliopata mimba na wakina mama waliozaa katika umri mdogo.

"WAZAZI WANAHITAJI KUWAFUNZA WATOTO UMUHIMU WA ELIMU NA INABIDI WAAMBIWE KUSOMA KWA BIDII. PIA, WAWAELIMISHE JUU YA MADHARA YA MIMBA ZA UTOTONI."

"WAKINA MAMA VIJANA INABIDI WAFUNZWE MALEZI BORA ILI WAWEZE KUWAKUZA WATOTO WAO VYEMA."

"WASICHANA WANAHITAJI KUPENDWA NA KUPEWA MSAADA WA HALI KUTOKA KWA JAMII BADALA YA KUTENGWA KWA KUWA TU WALIPATA MIMBA KATIKA UMRI MDOGO."

HITIMISHO

Utatuzi wa tatizo tata la akina mama waliozaa katika umri mdogo hauwezi kupatikana kwa mtu mmoja, bali inabidi kuwa na juhudi zilizoratibiwa na zinazofanywa na watekelezaji mbalimbali.

Ukosefu wa sera zilizoundwa na wizara kuwasaidia wasichana wenye ujauzito na akina mama waliozaa katika umri mdogo inabidi ufanyiwe kazi. Wakati huo huo, sheria zilizopo za kuwalinda watoto, hasa wasichana na wanawake waliozaa katika umri mdogo zinahitaji kutekelezwa kwa dhati.

Vijana inabidi wafundishwe kujiamini na kuboresha stadi zao za mahusiano ili waweze kujadili na kukataa ngono na ndoa za kulazimishwa. Programu maalumu zianzishwe na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasaidia vijana wasio shuleni na wakina mama waliozaa katika umri mdogo kukuza stadi zao za biashara na ujasiriamali.

Wazazi na walezi wahamasishwe kuwaelimisha watoto wao juu ya afya ya uzazi na kuwapa mahitaji ya msingi, ikiwa ni pamoja na kulipa ada ya shule na kununua vifaa vya elimu. Huduma za afya inabidi zipanuliwe ili kutoa taarifa juu ya mimba za utotoni na hatari zake, matumizi ya uzazi wa mpango, utoaji mimba na matatizo yake, na madhara ya kuzaa katika umri mdogo.

“NAHITAJI KURUDI SHULE ILI HAPO BAADAE NIWE NA KAZI NZURI. KUWA MAMA ALIYEZAA KATIKA UMRI MDOGO SIO MWISHO WA NDOTO ZANGU.”

ukwaa la Utu wa Mtoto (CDF)ni shirika lisilo la kiserikali, lenye makao yake makuu Dar es Salaam, lililoundwa na kusajiliwa mwaka 2006 chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24/2002. CDF ina Ofisi nyingine mkoani Mara na Dodoma.

CDF hujishughulisha na masuala ya haki za mtoto kwa njia ya kushawishi mtazamo wa umma na sera, na kujenga uwezo (juu ya sheria na haki za binadamu) wa mashirika yanayolenga watoto nchini Tanzania. Ni jukwaa la mazungumzo na majadiliano juu ya masuala yanayowaathiri watoto. Inalenga kuangalia masuala mapya na mijadala inayowahusu watoto. CDF "huwaweka watoto KWANZA" katika vipengele vyake vyote vya kazi.

Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF)
S.L.P 34241,
Eneo la Mwenge,
Kiwanja Na..161/162,
Ghorofa ya Pili, Jengo la Mama Ngoma
Dar es Salaam

Simu: +255 22 2775010
au +255 743 902858
www.cdftz.org
Facebook: facebook.com/cdftz
Twitter: @cdftz
Instagram: @cdf_tanzania

FORWARD ni shirika la haki za wanawake linaloongozwa na Waafrika. Kazi zetu zinalengamasuala yanayohusu ukeketaji kwa wanawake, ndoa za utotoni, na aina nyingine za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ambao unaathiri afya, utu na ustawi wawanawake na wasichana wa Kiafrika.

Tunafanya kazi na wanajumuiya, wataalamu, watunga sera, na kupitia mitandao na ushirikiano wa kimkakati. Hii inatuwezesha kupaisha matokeo ya kazi zetu katika sehemu mbalimbali.

Ndotoyetu nikufikia siku ambapo mwanamke wa Kiafrika atapata haki na fursa sawa, ataudhibiti mwili wake na kutokabiliwa na ukatili.

FORWARD
Suite 4.7, Chandelier Building
8 Scrubs Lane, London
NW10 6RB, UK

Charity Number: 292403

Simu: +44 (0) 20 8960 4000

www.forwarduk.org.uk
Email: forward@forwarduk.org.uk
Facebook: facebook.com/FORWARDUK
Twitter: @FORWARDUK